# MATUKIO YA MWEZI APRILI SUA

**"Ardhi ni Hazina"**

## YALIYOMO



WAZIRI NDALICHAKO ATAMBUA MCHANGO WA SUA KATIKA MASUALA YA KILIMO.

UK.1-2



SERIKALI YAAHIDI KUKARABATI KARAKANA ZA UHANDISI KILIMO CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO (SUA)

UK. 3-4



PROF. GABRIEL AFURAHISHWA NA HOSPITALI YA RUFAA YA WANYAMA SUA

UK.5-6



WAWAKILISHI WA MASUALA YA JINSIA WAPEWA MAFUNZO YA KUZUIA UNYANYASAJI MAHALI PA KAZI.

UK.7

# MATUKIO YA MWEZI APRILI SUA

**"Ardhi ni Hazina "**

## WAZIRI NDALICHAKO ATAMBUA MCHANGO WA SUA KATIKA MASUALA YA KILIMO.

Waziri wa Elimu Sayanasi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako amesema Serikali kupitia Wizara yake imeendelea kukiimarisha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ikitambua juhudi zinazofanywa na sua kuandaa wataalamu wa kilimo.

Waziri Ndalichako aliyasema hayo mkoani Morogoro wakati wa kufunga wiki ya Kumbukizi ya Hayati Edward Moringe Sokoine iliyoanza tarehe 9 Aprili na kumalizika tarehe 12 Aprili, 2019 katika Kampasi kuu ya SUA.

***"Kwa kuweka msisitizo katika kilimo na hii ni kwa sababu asilimia kubwa ya Watanzania ajira yao ni kilimo na kwa kuwa leo tupo katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine nitazungumzia mambo ambayo Serikali inayafanya katika kuimarisha kilimo chetu kwa kuwa kilimo bora kinatakiwa kuwa na utaalamu bora na hiki ndio chuo mahususi katika nchi yetu kwa sasa cha kuandaa wataalamu wa kilimo".alisema Ndalichako.***

Aidha aliongeza kuwa Serikali imekuwa ikiweka msisitizo katika ufundishaji wa masuala ya kilimo kwa nadharia na vitendo na Serikali imefanya mambo mengi katikia kuboresha mazingira ya kujifunzia katika chuo kwa kujenga Maabara ya Sayansi yenye uwezo wa kuchukuwa waanafunzi wapatao 400 na imekwisha kamilika na Maabara pamoja na vifaa vyake imegharimu bilioni 2 na milioni miatatu.

Waziri Ndalichako aliongeza na kusema kuwa, Kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia Chuo kimepokea kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya uboreshaji wa Maabara ya udongo iliyopo Chuoni hapo kwa ajili ya kutoa msaada kwa wakulima pamoja na wanafunzi wanaosoma masomo ya Kilimo.

***"Kupitia Tume ya Sayansi na teknolojia Chuo kimepatiwa sh milioni 400 kwa ajili ya kuboresha maabara ya udongo, wakati mwingine wakulima wetu mazao yanaweza yasiwe na tija kwa sababu wanajipandia .lakini kitaalamu afya ya udongo inaweza kuathiri uzalisha na mazao yanayoweza kupatika, kwa hiyo tunataka wanafunzi wanaomaliza hapa wakawe chachu huko wanakokwenda kwenye masuala ya kilimo"alisema ndalichako***

Pia kupitia Mradi wa kuendeleza ujuzi, Chuo kimepatiwa shilingi milioni mia tatu kwa ajili ya kuboresha mafunzo kwa vitendo, na imeahidi kutoa shilingi milioni 750 kwa ajili ya kuboresha Karakana ya Uhandisi kilimo.

Katika hatua nyingine Waziri Ndalichako ameelezea kufurahishwa na namna Chuo Kikuu cha Sokoine kinavyoendelea kumuenzi na kumpa heshima kubwa Hayati Edward Moringe Sokoine ambaye alikuwa shujaa,mchapa kazi ,mzalendo na mtu ambaye alijitoa katika kulitumikia Taifa na kwamba mpaka mauti yanamkuta alikuwa kazini.

*Inaendelea uk.2*

# MATUKIO YA MWEZI APRILI SUA

## "Ardhi ni Hazina "

### WAZIRI NDALICHAKO ATAMBUA MCHANGO WA SUA KATIKA MASUALA YA KILIMO.

*"Tunawajibu wa kuishi mazuri ambayo yamefanywa na kiongozi huyu,SUA nafurahi kuona mnawashirikisha wanafunzi katika midahalo hii vizuri wakajua taifa limetoka wapi, nchi hii imetulia kwa kuwa kuna watu walifanya kazi usiku na mchana ya kujenga amani umoja na mshikiamo. ni rahisi sana kufanya kitu kimoja cha kuvuruga amani na mshikamano lakini ikivurugika kuijenga inaweza kuchukuwa karne kuirudisha, kwa hiyo tuendelee kuwaenzi waasisi wa Taifa hili kwa kuyaishi waliyoyafanya" alieleza Waziri Ndalichako*







*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako akiwa kwenye picha mbalimbali wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Kumbukizi ya Sokoine.*

## SERIKALI YAAHIDI KUKARABATI KARAKANA ZA UHANDISI KILIMO CHUO KIKUU

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeahidi kutoa jumla ya Tsh. 750 milioni kupitia mradi wa kukuza ujuzi na stadi za kazi (ESPJ) ili kukarabati karakana mbalimbali hasa zile za uhandisi kilimo.

Akizungumza wakati akifungua rasmijjuma la Kumbukizi ya Sokoine Dkt. Leonard Akwilapo amesema kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kina mchango mkubwa katika azma ya kuleta mapinduzi katika Kilimo hivyo ukarabati wa karakana hizo una dhumuni la kumuenzi Hayati Edward Moringe Sokoine.

***"Katika siku hii ya kihistoria Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itakiunga mkono Chuo kwa kufanya ukarabati mkubwa wa Karakana ili karakana hizi ziwe bora na ziendane na mwenye jina la Chuo, Hayati Sokoine" alisema Dkt. Akwilapo.***

Aidha aliongeza kuwa mada ya kumbukizi hili imejikita vyema katika mipango ya sasa ya serikali ya Awamu ya tano hususani dhana kuu tatu ambazo ni uzalishaji katika kilimo, mageuzi ya viwanda na maendeleo ya Tanzania na hivyo kuwataka wanataaluma kufanya uwasilishaji na mijadala mizuri ya maandiko katika mkutano wa kisayansi ili kuwa na mipango mizuri kwa mustakabali wa baadaye kwa kuangalia matokeo ya maadhimisho ya mwaka huu ya kifo cha Hayati Edward Moringe Sokoine.

Naye Makamu wa Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda alisema kuwa kumbukizi hili limekuwa ni chachu ya kuendeleza mambo mazuri aliyoyafanya Sokoine na kuhakikisha maono yake yanakuwa hai.



***Katibu Mkuu wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Dkt. Leonard Akwilapo akiapa maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Kudhibiti wanyama waharibifu Dkt. Ladislaus Mnyone.***

*Inaendelea uk.4*

# MATUKIO YA MWEZI APRILI SUA

**"Ardhi ni Hazina "**

## SERIKALI YAAHIDI KUKARABATI KARAKANA ZA UHANDISI KILIMO CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO (SUA)

***"SUA imekuwa ikifanya kumbukizi hili ikiwa ni kama sehemu ya kumuenzi Hayati Edward Moringe Sokoine kwa kuendeleza mambo aliyoyafanya na kufanya maono yake kuwa hai kwa ajili ya maendeleo ya Taifa", alisema Prof. Chibunda.***

Prof. Chibunda alisema pamoja na maonesho ya kazi za SUA pamoja na teknolojia pia kutakuwa na mdahalo wa kitaifa ambapo maarifa yatakayopatikana yatahaririwa kwa umahiri na umakini mkubwa na kuchapishwa kwenye toleo maalumu la Jarida la Kisayansi.

Itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 7 Mei, 2018 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. John Pombe Magufuli alitembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na kutoa matrekta 10 kwaajili ya mafunzo kwa vitendo ya wanafunzi na wananchi kwa ujumla. Hivyo basi ujio huu wa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na ahadi aliyoitoa inaonyesha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 yenye lengo la kuifanya sekta ya kilimo kuwa yenye ufanisi, ushindani na yenye kuleta faida ambayo itachangia kuboresha maisha ya Watanzania na hivyo kufikia uchumi mkubwa na kupunguza umasikini.





***Ziara za viongozi mbalimbali wakati wa Moonesho Wiki ya kumbukizi ya Hyati. Edward Moringe Sokoine.***



# PROF.GABRIEL AFURAHISHWA NA HOSPITALI YA RUFAA YA WANYAMA SUA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo Profesa. Elisante Ole Gabriel amefurahishwa na shughuli zinazofanywa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo hususan uwepo wa Hospitali ya Rufaa ya Wanyama.

Hospitali hiyo ni taasisi pekee nchini inayosaidia kutoa ushauri, tiba na chanjo kwa wanyama wa kufugwa na waporini ambao wamepewa rufaa kutoka katika Hospitali ndogo ndogo za wanyama, taasisi za serikali na binafsi ambazo huhifadhi na kuwatunza wanyama hao ambao hupatikana kisheria.

Akizungumza wakati wa ziara yake ya siku moja chuoni hapo leo Aprili 23, 2019, Prof. Gabriel amesema alipata fursa ya kuzunguka nchi za Afrika Mashariki lakini hakuwahi kusikia uwepo wa Hospitali ya Rufaa ya Wanyama na hivyo kuwataka waandishi wa habari kwa kushirkiana na kitengo cha Mawasiliano na Masoko kuhakikisha Umma unafahamu kuhusu Hospitali hiyo kuwepo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

***“Nimefurahishwa na Hospitali ya Rufaa ya Wanyama hapa SUA ambayo ni kwa Tanzania nzima, ni vyema tukauhabarisha Umma kuhusu hili na ikibidi Waziri aweze kutembelea Hoapitali hii, kiukweli nimefurahishwa sana na mambo niliyoyaona hapa SUA na nashukuru ziara yangu hii sikukosea kuifanya hapa”. Alisema Prof. Gabriel.***

Pia aliongeza kuwa SUA inaweza kuwa zaidi ya eneo la mafunzo kwani kuna utalii ndani yake ambapo aliwashauri watumishi wa Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya kuanzisha programu ya Utalii ambapo watu wakija kufanya mafunzo ya tiba ya wanyama wapate kujionea mambo ya Utalii yaliyopo katika Ndaki hiyo na hata Ndaki nyingine.

Aidha, Prof. Gabriel alipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya Hospitali hiyo na kujionea shughuli zinazofanywa ambapo alipata fursa ya kuona wanyama wakipatiwa tiba ikiwemo upasuaji wakiwa katika uangalizi wa madaktari maalum wa wanyama.

Inaendelea Uk 6

# MATUKIO YA MWEZI APRILI SUA

## *"Ardhi ni Hazina "*

***"Sikuwa najua kama paka anaweza akafanyiwa upasuaji na kukatwa mguu na bado akaendelea kuwa hai hivyo natoa wito kwa wananchi wote kutumia Hospitali hii kuleta wanyama wao ili waweze kupatiwa matibabu mbalimbali, mimi nimefanikiwa kuona paka aliyefanyiwa operesheni na kukatwa mguu pamoja na mbwa ambao wote wako katika hali nzuri", alisema Prof. Gabriel.***

Katibu Mkuu huyo pia alipata fursa ya kuzungumza na Menejimenti ya Chuo na kuwataka kuendelea kuzalisha wahitimu bora na kuwafanya kuwa ni wahitimu waliofundishwa kwa vitendo zaidi kuliko nadharia huku akishauri kuwa Chuo kitoe uelewa kwa wanafunzi kuwa sekta ya mifugo ni sekta inayoajiri zaidi ya asilimia 50 ya wataalam wa mifugo na kutambua kuwa ni vyema wajijengee hari ya kutaka kujiari ili nao waweze kuja kuajili wengine pia.

***"Ili tumuenzi Rais wetu John Pombe Joseph Magufuli ambaye ameonyesha msukumo wa pekee ni vyema tuhakikishe wahitimu wetu wanakuwa na uelewa kwa vitendo na si nadharia tu ili kutatua changamoto za wanafunzi", alishauri Prof. Gabriel.***

Aliongeza kuwa chuo kinatakiwa kuongeza nguvu katika kutoa mafunzo ya biashara (Business knowledge) hususan katika upande wa tiba ya wanyama na Sayansi ya wanyama ili kuwapa wataalam ujuzi wa masuala ya biashara.

***"Nina hakika tukiongeza mafunzo ya biashara kwa wataalam wetu itasaidia kupata wanafunzi wa tofauti sana ambao mara baada ya kumaliza Chuo wakienda mtaani hawatapwaya katika utendaji kutokana na taaluma waliyopewa kwani biashara ndio kila kitu", aliongeza Prof. Gabriel.***

Prof. Gabriel amesisitiza Chuo hicho kihakikishe kinawagusa wafugaji wa chini kwa kushirikiana na Wizara kuwapeleka wanafunzi kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika sehemu halisia za kujifunzia.

***"Chuo kishirikiane na Wizara pamoja na Tamisemi kuandika barua ili kuomba Wilaya mbalimbali zikubali kuwapokea wanafunzi wetu na kuwapatia maradhi badala ya kuwaacha wanafunzi hao kwenda mahali ambapo hawatapata nafasi ya kujifunza kwa vitendo wakijaribu kukwepa gharama za kujihudumia wawapo katika mafunzo na hivyo kuangalia wapi wana jamaa ambao wanaweza kupata hifadhi", alisisitiza.***

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chubunda alimshukuru Katibu Mkuu kwa ujio wake na mchango wa mawazo ambapo alisema kwa kiasi Chuo kimeshaanza kushughulikia baadhi ya masuala hususani kuwa na mahali halisia pa kujifunzia na hivyo kuanzisha mashamba darasa ya mazao ya kimkakati kwa ajili ya wanafunzi na jamii kwa ujumla.

***"Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Mgufuli kwa kuwekea mkazo uwezeshaji kwenye vyuo na hasa chuo chetu kwa miaka miwili iliyopita kuna mambo makubwa ambayo huko serikali ilikuwa kama imevisusa vyuo vyake na kubaki kama yatima na kusababisha kuchakaa kwa baadhi ya miundombinu ya kufundishia mfano chuo chetu tunategemea mashamba na karakana ambazo kwa sehemu kubwa zilichakaa. Kwa sasa serikali na menejimenti ya chuo imefanya juhudi ya kupata mashamba makubwa ya chuo yaani "Modal farms na tumepanda mazao yote ya kimkakati kama vile zabibu, korosho pamoja na chai" alisema Prof.Chibunda.***

Aidha, katika kuimarisha utoaji wa elimu bora Chuo kimeboresha maeneo ya mifugo kama vile ngombe, samaki na maabara kwa lengo la wanafunzi kujifunzia kwa vitendo.

# MATUKIO YA MWEZI APRILI SUA

## "Ardhi ni Hazina"

## WAWAKILISHI WA MASUALA YA JINSIA WAPEWA MAFUNZO YA KUZUIA UNYANYASAJI MAHALI PA KAZI.





Wawakilishi wa masuala ya jinsia katika Chuo Kikuu cha Sokoine Cha kilimo SUA,wamepewa mafunzo ya wakufunzi juu ya kuzuia unyanyasaji wa kijinsia mahali pa kazi yaliyotolewa na Mkurugenzi wa Martha Farrell Foundation Memorial Fellow Bi.Nabdita Bhatt.

Mafunzo hayo ya siku mbili yaliandaliwa na Kamati ya Utekelezaji wa sera ya Jinsia ya Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo,SUA, kwa kushirikiana na Dkt.Fatihiya A. Masawe.

Mafunzo hayo yalilenga kujenga uwelewa wa pamoja kuhusu unyanyasaji wa jinsia,kujenga uwezo wakati wa kuendesha mafunzo kwa kutumia njia ya ushirikishwaji pamoja na muda ulipangwa katika utekelezaji wa sera.

Mafunzo yalihusu hasa masuala ya unyanyasaji wa kijinsia katika kampasi zote za SUA.

Washiriki waliweza kufanya kazi kwa vikundi na kutoa mawasilisho juu ya mambo mabali mbali kama vile ni kwanini wanahitaji kuwa na uwelewa wa masuala hayo na wanatarajia kufanya nini mara baada ya amafunzo hayo.

Jumla ya washiriki 30 kutoka vyama vya wafanyakazi,wanafunzi pamoja na watoa huduma wa SUA walishiriki Mafuanzo hayo.